Hekima ya Swalah ya jamaa na Fadhla zake

1. Kujuana kwa ndugu na wanaopendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wao kwa wao na kutilia nguvu ushikano wa mapenzi baina yao, mambo ambayo imani haiwi isipokuwa kwa hayo. Kwani hakuna njia ya Imani wala ya Peponi isipokuwa kwa kupendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka.

2. Kuepukana mja na unafiki na Moto kwa aliyewahi takbiri ya kufungia Swala siku arubaini mfululizo, kwa hadithi aliyoipokea Anas kutoka kwa Mtume ﷺ: (Mwenye kuswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu siku arubaini kwa jamaa, akawa anawahi takbiri ya kwanza, ataandikiwa kuwa mbali na Moto na kuwa mbali na unafiki) [Imepokewa na Tirmidhi.].

3. Kukusanyika waislamu walio huku na kule na kuzizoweza nyoyo zao kheri na utengefu.

4. Kushikamana Waislamu na kusaidiana kwao baina yao.

5. Kudhihirisha ibada za Dini na nguvu yake.

6. Kuziunganisha nyoyo za Waislamu, kwa kumfanya mweupe na mweusi, Mwarabu na asiyekuwa Mwarabu, mkuu na mdogo, tajiri na masikini, wote wakawa pamoja ndani ya msikiti mmoja, nyuma ya imamu mmoja na katika wakati mmoja, wote wanaekelea kibla kimoja na muelekeo mmoja.

7. kuwatia hasira maadui wa Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa Waislamu bado wana nguvu iwapo wataendelea kutunza utekelezaji Swala misikitini.

8. Kufutiwa dhambi na kupandishwa daraja. Imepokewa na Abu Huraira t kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: (Je si niwajulishe kitu kinacho sababisha kufutiwa dhambi na Mwenyezi Mungu na kupandishwa daraja? Wakasema: “Kwani? Tujulishe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu” Akasema: “Nikueneza maji ya kutawadhia kwenye viungo, na kuwa na hatua nyingi za kwenda msikitini, na kungoja Swala baada ya Swala. Kwani huko ndiko kujitolea katika kusimamisha Dini) [Imepokewa na Muslim.].

9. Swala ya jamaa ni bora kuliko Swala ya mwenye kuswali peke yake kwa daraja ishirini na saba. Ibnu ‘Umar t amepokewa kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: (Swala ya jamaa ni bora kuliko Swalah ya mwenye kuswali peke yake kwa daraja ishirini na saba) [Imepokewa na Bukhari.]

Chanzo cha: https://www.al-feqh.com/sw/swala-ya-jamaa

al-feqh.com/sw